HII NI HOTUBA maalum iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Javier Perez De Cuellar, kuhusu maadhimisho ya Sikukuu ya Miaka Arobaini ya Umoja wa Mataifa mwaka huu 1985. Imehaririwa na Mhariri wa Kiswahili, Bw. Abdulrahman Sheriff.

# UMOJA WA MATAIFA WATIMIZA MIAKA 40 TANGU UANZISHWE

na J.P.D. CUELLAR

NI MIAKA arobaini tangu Ulimwengu ushuhudie kuwekwa kwa msingi wa Shirika jipya la kujenga ushirikiano wa Kimataifa. Shirika hili limekua sana katika kipindi hiki, na kazi zake zimezidi kushughulikia matatizo ya karne yetu.

Huku ikipitia misukosuko ya kipindi hiki, Shirika la Umoja wa Mataifa limeweza kukumbatia karibu watu wote wa dunia yetu, pamoja na mawazo na mashaka yake.

## MAAFA

Ingawa shirika hili limekabili matatizo mengi, limejitahidi kuwalinda wasio na chochote na kuwaletea msaada waliokumbwa na maafa.

Shirika hili limeonyesha njia ya kuleta amani ulimwenguni kwa kueleza misingi ya tabia njema za jamii ya kimataifa zinavyopasa kuwa na kuonyesha kwa vitendo kinachofaa kufanywa ili kurekebisha hali mbalimbali zisizofaa.

Kwa kufafanua kanuni za kuhakikisha haki za binadamu, shirika hili limetegemesha wazo la heshima kwa wanadamu. Mataifa yameunganika kwa njia ambazo hazijawahi kuwako na mpaka wa sheria ya kimataifa umezidi kupanuka.

Shirika hili limesaidia kuelimisha watu wote kuhusu umuhimu wa kurekebisha mwenendo wa ushirikiano wa kiuchumi kati ya mataifa mbalimbali ili kuwe na maendeleo ya kulinganika katika sehemu zote za ulimwengu.

Kabla ya kuanzishwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa, wazo la kuwa na jamii ya kiulimwengu lilikuwa kama ndoto. Lilipozaliwa shirika hili, wazo hili sasa limekuwa ni ukweli wa maisha yetu. Hatua kubwa imechukuliwa katika maendeleo ya siasa ya binadamu.

*HATA hivyo, uhakiki wake utategemea wakati Mataifa hayataendelea kugombana na kupigana, wakati sheria na tabia zinazoeleweka zinavutia utii wa mataifa yote, wakati jamii ya binadamu imekuwa huru kutoka hofu ya kuangamizwa na mabomu ya 'Nuclear' na wakati sehemu kubwa za ulimwengu hazitabakia kwenye hali ya kukosa tumaini sababu ya umaskini na kutokujua.*

Kwa kweli, hili ni wazo kubwa mno, Lakini hata hivyo, wazo na ndoto ya karne iliyopita, leo imekuwa kitu cha lazima kama ustaarabu wa binadamu ulimwenguni utaendelea.

Hata kama vita, ugomvi na mashindano ya kukusanya vyombo vya vita zinasababisha hali ya kufa moyo kwa wengi, wazo hili kubwa ni lazima lichochewe na watu wote waendelee kukuwa na imani kuwa na uelewano zaidi kwenye shughuli zote za Kimataifa.

## KANUNI

Kinachoweza kuimarisha imani hii ni Shirika la Umoja wa Mataifa pamoja na nia na kanuni zilizoamsha na kuelekeza mkataba wake. Jitihada zinazofanywa ili kuleta amani, haki na heshima kwa binadamu wote ni jitihada za watu wote wa ulimwengu.

Binadamu wote wakiendelea kuhimiza na kusaidia jitihada hizi, kunaweza kuwa na msukumo wa maendeleo mbele, badala ya hali ya kurudi nyuma.

Binadamu wote wakiwa waaminifu na juhudi katika kusaidia kutekeleza malengo yanayosisitizwa na shirika hili, Umoja wa Mataifa unaweza kuwa chombo chenye nguvu zaidi cha kuonyesha mfano wa nia njema ya binadamu wote; chombo ambacho ulimwengu unaozidi kuwa na mabadiliko mengi ya kasi unahitaji sana.

Ninaweka wazo hili leo mikononi mwenu nyinyi wananchi wenzangu wa ulimwengu wetu.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

Wasafishaji mashuhuri wa picha za rangi za FUJI ulimwenguni sasa wanapatikana mjini Mombasa

Aina zote za picha za rangi zinachapishwa:
FUJI • KODAK • AGFA
SAKURA • COLOURAMA

KWA USAFISHAJI WA PICHA ZAKO ZOTE ZA RANGI HAKIKISHA UNAZITUMA KWA MITAMBO MIPYA YA KISASA YA FUJI

Zungumza na Riaz Alibhai kwa simu 313589, Mombasa ama fika kwenye mitambo hiyo mipya ya FUJI, iliyo pakana na afisi ya Coastweek, gorofa ya kwanza ya jumba la Banki ya Grindlays, katika barabara ya Digo Road na Nkrumah road.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

# Risala Maalum Kutoka Amu

*na Abdulrahman Sheriff*

MWENYEKITI wa KANU Wilayani Lamu, Diwani Ali Mahrus alipongeza hatua iliyochukuliwa na makao makuu ya chama ya kutayarisha Semina katika mikoa yote ili viongozi wa KANU wapate kushauriana katika mambo kadha yanayohusiana na chama.

Akizungumza na mimi wakati wa ziara yangu mjini Lamu, Diw. Mahrus aliye pia mwenyekiti wa baraza la Lamu aliniambia kwamba Semina kama hizo zinahitajika kila wakati ili viongozi wapate kupeane mawazo ya busara ya kukiimarisha chama.

Diw. Mahrus akaongeza: "ni juu yetu sote viongozi tuliohudhuria semina hiyo kuzingatia maongozi ya chama kwa kutilia nguvu amri zake na kufuata kwa vitendo katiba na maongozi ya chama katika kuwatumikia wananchi inavyotakikana".

Mwenyekiti huyo alipongeza Kanu wilayani Mombasa kwa matayarisho mazuri ya kuandaa semina hiyo. "Sina budi kumpongeza Mwenyekiti wa Kanu Mombasa, Bw. Sheriff Nassir kwa kututayarishia vyema na kutupokea vizuri tulipohudhuria Semina hiyo", akasema.

Diw. Mahrus alimwomba Waziri wa Mali ya Asili, Bw. Jeremiah Nyagah awaruhusu watu wa Lamu wakate mikoko na kutafuta masoko ya nje kwani alisema, "mikoko yanaweza kuwapatia wanachi pesa za kutosha na pia Serkali kujipatia fedha za kigeni".

MBUNGE wa Lamu Mashariki, Bw. Mzamil Omar Mzamil pia alipongeza makao makuu ya chama kinachotawala cha Kanu kwa kutayarisha Semina katika kila mkoa nchini na akataja semina iliyofanyika Mombasa Kama "iliyofanikiwa sana".

Katika mahojiano na *Coastweek,* Bw. Mzamil alisema ni juu ya viongozi wote wa Kanu, Wabunge na Madiwani kuona kwamba wananchi wanatumikiwa na kutendewa ipasavyo.

"Utumishi wetu kwa wananchi waliotuchagua unahitajika kuwa wa kuridhisha", akaongeza Mbunge huyo.

Akigusia kuhusu hali ya mji wa Lamu, Bw. Mzamil alisema kwamba yale yanayoandikwa kwamba uchafu umetapakaa mji mzima yalikuwa ya kweli na akawa na maoni kuwa, "lazima hatua ya haraka ichukuliwe kabla ya maradhi mabaya kuchipuka".

Akisema kwamba hana nia ya kumshambulia yoyote, Bw. Mzamil alisema Baraza la Lamu lina jukumu kubwa la kufanya taratibu ili takataka zilizojaa zisafishwe na wananchi waishi maisha yanayostahiki.

Mbunge huyo akaongeza: "ikiwa Baraza limeomba lipatiwe msaada kutoka kwa Serkali Kuu na bado halijapatiwa, lazima litafute mbinu nyingine za kutafuta pesa ili kazi ya kuusafisha mji ianze mara moja na mji uonekane kuwa msafi".

Bw. Mzamil aliiomba Wizara ya Maji nayo ifanye taratibu za kumaliza tatizo la maji kwa wananchi wa mji huo. Alisema wananchi wa mji huo wamekumbwa na taabu ya maji kwa kipindi kirefu na sasa "umefika wakati wanahitaji tatizo hilo limalizwe".

Aliwasifu wananchi wa Lamu kwa utulivu na uvumilivu walionao na akawahakikishia kuwa, "Serkali yetu tukufu inawapenda wananchi wake na itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kuwa wanaishi maisha ya raha na furaha".

# SOUD A. KOKO

MWANAMUZIKI mashuhuri anayejitokeza kwenye *Coastweek* Ijumaa hii ni Bw. Soud Aly Koko, kiongozi wa bendi ya Zengela Ngoma.

Alianza kujishughulisha kwenye mambo ya muziki tokea mwaka 1970 alipounda bendi ya Ujamaa Jazz na kuibadilisha jina 1972 na kuiita Viva Vijana.

Ilibadilishwa tena jina mwaka 1979 na kuiita Viva Vijana.

Ilibadilishwa tena jina mwaka 1979 na kuitwa Les Viva hadi 1982 bendi hiyo ilipovunjika.

Ndipo Bw. Koko akuanda bendi yake mpya ya *Zengela Ngoma* ambayo inaendelea kuonyesha uhodari wake hadi sasa.

PICHA NA STORI: LAWRENCE M. MWANTHI

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI

HAKIKA
UTA FURAHI

## JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI

## CROSSWORD No. 221

*KWENDA KULIA:*

1. Mwizi atumiaye silaha. 5. Medical Officer. 6. Ni mzaa baba kisha ni tunda. 7. Umoja wa mataifa. 8. Namna ya embe. 9. Mnyama mkubwa mwenye umbo kama la paka. 10. Chimba udongo kama vile maji yanavyomomonyoa. 14. Kama No.7 kwenda kulia. 15. Utulivu. 17. Kivazi cha kike. 18. Asili ya tunda. 19. Tosha, pekee.

*KWENDA CHINI:*

1. Aina ya mdudu. 2. Kinyume cha bandika. 3. Zaidi. 4. Aina ya samaki wa bahari. 5. Wakati. 9. Kidonda kikubwa. 11. Mbaya. 12. Mti wa mtama. 13. Mjinga, mpumbavu. 15. Namna ya karata. 16. Weka ndani. 17. Afrika kusini.

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 220**

*KWENDA KULIA:* 1. KAMBARE, 5. LA, 6. MOMBASA, 9. DA, 10. AMUA, 11. UKAKASI, 13. KESI, 14. GUU, 16. UTU, 18. AM, 19. PANDA, 21. ALA, 22. TII. *KWENDA CHINI:* 1. KIMBUNGA, 2. BABAKE, 3. RISASI, 4. MAKANJU, 7. MDAKU, 8. AMI, 12. ASIA, 15. UMA, 16. UDI, 17. TAI, 19. PA, 20. NT.

**WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 220**

AMINA KANDIE, Sanduku La Posta 93044, Mombasa. 2. FRANCIS KALAITA MUNYALO, Sanduku La Posta 83987, Mombasa. 3. AHMED MOHAMED, Sanduku La Posta P.O. Box 81412, Mombasa.




JINA.................................................

SANDUKU LA POSTA.........................................

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK*, S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma Majibu na jumatano, **Desemba 4, 1985.** saa, nne asubuhi.

PONGEZI Wana wa Kwetu,
Kwa Nguvu ya Mola Wetu,
Na Subira Ndio Utu,

Ndio Hao Simba Ndume,
Yazingatie Upime,
Kuziata Nyemenyeme,

Dunia Ina Mazito,
Mfano wa Gai Moto,
Mtu Kuata Watoto,

Mumewaacha Watoto,
Jambo Ambalo ni Zito,
Mukaivuka na Mito,

Miwili au Mitatu,
Kwa Mungu Hilo sikitu,
Gongagonga na Kukutu,

Enyi Kina Dada Bora,
Izidisheni Subira,
Mutaipata Tiiara,

Mulioko Arabuni,
Mungu awape Makini,
Hadi Kurudi Mjini.

Wastahamilio Mambo,
Usije nitia Kombo,
Kuepuka Urembo.

Ndugu Zangu Fikirini,
Likitetelewa Kuni,
Akafika Arabuni.

Na Mke Aliye Nyumbani,
Mukangia Safarini,
Miyaka Hamuwaoni.

Miyaka Mukatimiza,
Zidini Kujichecheza,
Si Mkao Wa Baraza.

Skikeni Dhamana Zenu,
Mungoje Waume Zenu,
Dunia na Akhera Yenu.

AA. K. AL-GHRAAB, Box 98690-MAJENGO LIBATI.